

Wizara kutekeleza mradi kabambe wa samaki

Na Penina Malundo

■ ■ WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema ili kukidhi mahitaji ya samaki nchini imeanza kutekeleza mradi wa matotolesho ya vifaranga vya samaki kupitia mradi wa usimamizi wa uvuvi wa Kanda ya Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SwioFish), ambao utasaidia kuchochea uchumi wa viwanda.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika maonyesho ya Sabasaba, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah alisema, mradi huo utasaidia kuibua sekta yau uvuvi na viwanda na kutoa fursa ya wanafunzi kujifunza kwa vitendo.

Alisema, mradi huo utasaidia

kukuza sekta ya viwanda na uvuvi na kutoa elimu kwa wanafunzi ambao watapata fursa ya kujifunza kwa vitendo.

Tamatamah alisema, kukamilika kwa mradi huo utachochea ongezeko la samaki hapa nchini na kukuza uchumi wetu.

Aliongeza kuwa, tayari mchakato wa ujenzi wa maabara Kunduchi umeanza ambapo watashirikiana na Chuo Kikuu na baada ya miezi mitatu ujenzi utaanza.

Tamatamah alisema, hapo awali tegemeo kubwa la samaki lilikuwa ni maji halisi, lakini kwa sasa teknolojia za kisasa zimesaidia kupata samaki wengi kwa ajili ya mahitaji.



W
Na
Luc

■ ■
kute
upin
wa l
wa
Mae
ame
na C
wilay
W
katik
Kijiji
Kafa
Ak
huo.
hum
sual
uzito
safar

Kaimu Kamishna Msaidizi wa umeme wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Innocent Luoga (wapili kulia), kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Huduma na Ufundi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Jones Olotu, na Kushoto ni Meneja Uzalishaji Umeme na Masoko wa Mamlaka ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Nda'ndzi Kiboko, walipofanya ziara ya kukagua kazi ya usambazaji wa umeme iliyofanywa na kampuni hiyo katika vijiji sita vya Wilaya ya Uyole mkoani Mbeya, juzi. Na Mpagapa na Wotul

NARCO yalalamikia uvamizi katika maeneo yake

Na Omary Mngindo, Fukayosi

■ ■ RANCHI ya Taifa (NARCO) inayopakana na vijiji vinavyounda Kata za Vigwaza, Fukayosi na Talawanda wilayani Bagamoyo Mkoa wa Pwani melalamikia uvamizi wa maeneo yao unaofanywa na wananchi wakushinkiana na baadhi ya viongozi.

Uvamizi huo unathibitishwa na uwepo wa mawe yaliyopandwa ndani ya hifadhi hiyo, ambapo walengwa wameuziwa kisha kumilikishwa kwa kufuata tatatibu huku kazi hiyo ikifanyika ndani ya eneo linalomilikiwa kisheria na serikali kupitia Wizara ya Mifugo

na Uvuvi.

Hayo yalielezwa na Meneja wa Ranchi hiyo, Elisa Binamungu mbele ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega, alipotembelea Vijiji vya Fukayosi na Mkenge Kata ya Fukayosi, kuzungumza na wananchi wanaolalamikia kukosa maeneo huku ikidaiwa kuwa ranchi hiyo imechukua maeneo yaliyopangiwa matumizi bora ya ardhi.

"Ili eneo lote linamilikiwa na Hifadhi ya Narco, humo utatembelea zaidi ya kilometa mbili mpaka nne uko ndani ya msimu huku kukiwa na mawe yaliyopandwa ikonesha ni maeneo

yanayomilikiwa na watu binafsi zikiwemo taasisi mojawapo Kanisa la Kiingili la Kirutheri Tanzania (KKKT)," alisema Binamungu.

Baada ya maelezo hayo, Wazin Ulega akamuagiza Mkuu wa Wilaya, Zainabu Kawawa apate majina ya wanaomiliki ardhi hiyo kisha kumfikishia ofisini kwake ili hatua za kisheria zichukuliwe kwani mbali ya kuzimiliki lakini hawazindelezi, wakati wafugaji wanagombana na wakulima.

Aliongeza kuwa katika hifadhi hiyo, zimetengwa hekta 20,000 kwa ajili ya kuwekwa vitalu vitavyotumiwa na jamii ya wafugaji wachungie mifugo yao, ili kuondoa migongano kati yao na

wakulima na kwamba mpango huo umeandaliwa na serikali chini ya Rais Dkt. John Magufuli.

Kwa upande wake, Kawawa alisema amepokea maagizo hayo na atayafanyakazi mapema iwezekanavyo huku akimpa wiki moja Mwenyekiti wa Kijiji aorodheshe majina ya wamiliki hao yamfikie ofisini kwake.

Naye Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, Dkt. Shukuru Kawambwa alishukuru serikali kwa kukipa kijiji hicho ekan 100 za ardhi huku akimuomba, Rais Magufuli afikine namna ya kuwaongezea kwani ndani ya ekan hizo tayan kina wananchi wanaofanya shughuli mbalimbali.